Mpende Jirani yako.

TAFADHALI BIBLIA YAKO IWE IMEFUNGULIWA NA UJARIBU KUTAFUTA KUMBUKUMBU REJEA ZOTE.

Katika somo hili tutatilia mkazo juu ya agizo la Yesu kwamba ikiwa kweli tunataka kuwa wanafunzi wake, tunapaswa kuonyesha katika maisha yetu upendo wa kupita kiasi kwa watu wengine.

Mahali pa kuanzia katika somo hili ni mfano uliotajwa katika somo lililopita, msamaria Mwema. Tukiangalia kwa makini maneno ya Yesu katika Luka sura ya 10 mistari ya 30 hadi 37 tunaona mambo mengi muhimu. Kwanza, kwamba Yesu alimchagua Msamaria kumweka katika mfano huu kwa kuwa Wasamaria walichukiwa na Wayahudi, walidharauliwa kama watu duni. Pili, kwamba mtu aliyeshambuliwa na wezi hakusaidiwa na watu wawili ambao ndiyo wangalikuwa wa kwanza kumsaidia. Kwa kuwa Makuhani walitoka katika kabila la Lawi wakati wa Sheria za Musa waliopaswa kutoa huduma za afya na masaidiano mengine kuwaangalia watu wa Israeli kwa jumla.

Alikuwa ni Msamaria aliyeonyesha upendo na huruma na alionyesha mambo haya ya msaada kwa vitendo. Alisafisha majeraha, alimchukua mtu aliyeumia juu ya punda wake na kumpeleka mahali pa usalama ili apumzike. Mwisho alikuwa ni yeye aliyewezesha mtu aliyeumia baadaye kupata mahitaji yote muhimu yaliyotakiwa.

Tunaposoma katika Injili kuhusu matendo mengi ya kuponya yaliyofanywa na Yesu, mara nyingi mwandishi anamalizia kwa maneno “Na Yesu alikuwa na huruma” kwa mtu mgonjwa au katika kisa cha kijana aliyefariki, kwa mama yake aliyekuwa na majonzi. Angalia Luka sura ya 7 mistari ya 11 hadi 15.

Mara baada ya Yesu kuchagua Wanafunzi wake kumi na wawili alianza kuwafundisha masomo ya upendo, msamaha na huruma.

Sasa ukifungua katika Biblia yako katika Luka sura ya 6 mstari wa 17, tutaangalia pamoja mambo haya. Umati wa watu uliokuwa ukimsikiliza Yesu siku ile ulikuwa mkubwa sana na walikuwa wametoka mbali sana kuja kumuona. Wengi wao walikuja ama kuponywa au kuona vitendo vya Yesu akiponya. Aghalabu walikaa

kusikiliza mafundisho yake juu ya Utume wa Mkristo na tutafanya vivyo hivyo tukitilia mkazo katika mistari ya 27 hadi 36.

Hakuna mwingiliano kwamba yale tunayoyasoma katika Injili ya Luka karibu ni yale yale tuliyoyasoma katika Injili ya Mathayo katika somo letu lililopita. Habari hii ni muhimu sana katika Biblia. Linaloanza kama wazo katika fikira zetu mara nyingi linageuzwa kuwa kitendo, hivyo sheria za Yesu hazina budi kwanza kutawala mawazo yetu. Tunapoonyesha upendo na huruma kwa mtu mwingine, tunafanya hivyo kwa vitendo.

Mara kabla ya Yesu kuondoka katika chumba cha juu alikokuwa akifurahia chakula cha mwisho na Wanafunzi wake kabla ya kifo chake, alirudia amri hii kuu kuhusu upendo. Tunaikuta katika Injili ya Yohana sura ya 13 mistari ya 34 hadi 35. Maneno yake yanahitaji mawazo makini kwani upendo wa Mkristo unaoonyeshwa na Wanafunzi wake hauna budi kuwa mkubwa kama ule ulioonyeshwa na Yesu kwa wanaume na wanawake wale katika nyakati zake na wote watakaomfuata kupitia historia. Alionyesha upendo wake kwa kukubali kufa katika msalaba ili wafuasi wake wote watakaoonyesha imani ya kweli wangekuwa na nafasi ya kuwa na maisha ya milele katika Ufalme wake katika dunia hii. Angalia katika Yohana sura ya 15 mistari ya 9 hadi 14 na ona jinsi amri hii ilivyorudiwa katika mstari wa 12 na mstari wa 17.

Wakati Petro alipopinga kuwa asingethubutu kumkana Yesu, Yohana sura ya 13 mistari ya 36 hadi 38, Yesu alimwambia kwamba kabla ya alfajiri kabla ya jogoo kuwika utamkana Bwana wako mara tatu. Haya yalipotokea sawasawa kama Yesu alivyotabiri, Petro aliaibika, lakini alijifunza somo la kwamba chakula aina ya mkate na samaki kumpenda Bwana wake halikuwa jambo rahisi kulitelekeza unapokuwa katika shinikizo.

Baada ya ufufuko wake, Yesu alikutana na Wanafunzi wake katika Galilaya ya Kaskazini ambako miongoni mwao saba waliamua kuchukua mtumbwi na kwenda kuvua samaki. Waliungana na Yesu katika Pwani ambako alikuwa ameandaa – Yohana sura ya 21 mstari wa 9. Ni muhimu kuelewa kuwa Yesu alionyesha huruma yake kwa umati wa watu elfu tano na baadae elfu nne kwa miujiza kuwalisha mikate na samaki.

Baada ya chakula katika Pwani ya bahari ya Galilaya, Yesu alimalizia somo la Upendo kwa kumuuliza Petro mara tatu kuhusu upendo wake kwa Bwana wake. Yesu aliongeza maneno mpya katika maagizo yake ya awali – mistari y 15 hadi 17; aghalabu mara kwa mara Petro aliposema anampenda Yesu alipewa agizo na majukumu "lisha kondoo wangu" ,"lisha kondoo wangu".

Katika miaka ya mwanzo ya Kanisa jipya, kulikuwa na kondoo wengi (wanafunzi wapya) waliotakiwa kuangaliwa. Kadri makanisa mapya yalivyoanzishwa katika sehemu nyingi za Israeli na nchi nyingine, vivyo hivyo majukumu yalibadirika na kwa hiyo ilikuwako haja ya kuyaangalia makundi yaliyokuwa yameanzishwa (Kondoo). Paulo alitumia lugha ile ile katika ujumbe wake wa kuagana na wazee wa kanisa la Waefeso – tazama Matendo ya Mitume sura ya 20 mistari ya 28 na 29.

Mtume Yohana pia alijifunza somo hili la maana la Upendo kutoka kwa Yesu. Akiwa ametundikwa katika msalaba, Yesu alimwambia na kumkabidhi majukumu juu ya mama yake Maria. Utayakuta haya katika Injili ya Yohana sura ya 19 mistari ya 26 na 27.

Takribani miaka 50 baadae, Yohana aliandika waraka ambao alitarajia kusomwa na makanisa yote. Katika waraka huo alielezea tu sheria ya Upendo wa Wakristo. Tafuta waraka wa kwanza wa Yohana na angalia katika sura ya 4 mistari ya 7 hadi 21. Soma haya kwa uangalifu kwani yana umuhimu wa pekee katika nchi ambako kuna chuki ya kutisha kati ya sehemu moja ya jamii na nyingine, kichaa cha mauaji ya halaiki cha kutaka kuteketezwa kati ya kabila na kabila. Vita kati ya sehemu moja na nyingine, mji na mji, kijiji na kijiji. Chuki na uchungu kati ya ukoo na ukoo. Maneno ya Yohana ni ya dhati na hayana mashaka katika mawazo ya watu. Haiwezekani kuwa Mwanafunzi wa Kristo kusema kwamba tunampenda Mungu wakati huo huo kuwachukia Wakristo wenzetu katika mioyo yetu. Kama mtu atasema anampenda Mungu na kumchukia ndugu yake ni mwongo. Haiwezekani kuyaepuka maneno haya, na kwa wale wanaotaka kubatizwa au wale waliobatizwa karibuni, hili ni somo muhimu.

Kwetu sisi kuna mambo mengi muhimu ya kukumbukwa kutoka katika maneno haya ambayo ningependa kuyatumia kwa uangalifu kama kumbukumbu ya somo hili.

1. Mstari wa 7 "Upendo ni wa Mungu" hii ina maana kwamba wakati wa uumbaji, uwezo wa kutokujipenda ulijengwa kwa mapenzi ya Mungu. Anatutaka tuitikie wito wake wa Upendo na Upendo wa Yesu kwetu sisi.
2. Mstari wa 10 Mungu alimtuma Yesu kama dhabihu kwa ajili ya dhambi zetu. Hiki ni kipimo cha Upendo wake kwetu sisi.
3. Mstari wa 11 kwa sababu Mungu anatupenda, tunapaswa kuonyesha upendo kwa wengine.
4. Mstari wa 12 – Tunapoonyesha upendo huu tuliopewa na Mungu kwa wengine, kuna jambo ambalo ni la Mungu ndani yetu.
5. Mstari wa 17 – Tunapoweza kwa dhati kuhisi kwamba tunao uwezo wa kuonyesha upendo tuliopewa na Mungu kwa wengine, hatutakuwa na hofu ya hukumu wakati wa kurudi kwa Yesu.
6. Mstari wa 18 – "Upendo kamilifu unaondoa hofu". Kuna manufaa ya uhakika kwa wale wanaoweza kuonyesha upendo wa aina hii.
7. Mistari ya 20 na 21: Hivi ni vifungu tulivyoviangalia tayari lakini kwa sababu ya ongezeko la mauaji na uadui kati ya watu katika nchi nyingi duniani, nataka kutilia mkazo umuhimu wa ujumbe huu. Hatuwezi kumpenda Mungu na kumchukia ndugu yetu. Kwanza kabisa Yohana anazungumzia kuhusu Wanafunzi wa Yesu waliobatizwa, hakuna udhuru ya uadui kati yetu. Kama jirani ya mtu, katika mfano wa Yesu, alikuwa Msamaria, vivyo hivyo jirani yetu anaweza kuwa mtu yeyote anayehitaji msaada wetu. Katika maana pana zaidi ya majirani kuwa ni watu tunaokutana nao kila siku, tuna kazi kubwa mbele yetu. Kwa bahati nzuri hatuna haja ya kujiingiza katika mambo ya watu wanaotupita kila siku lakini tukifanya hivyo amri ya Yesu sharti ikumbukwe. "Mpende Mungu na jirani yako kama unavyojipenda mwenyewe.

CBM Publishing, 32 Blenheim Rd, Far Cotton, Northampton NN4 8NW United Kingdom
PO Box 2950, Mbeya, Tanzania (East Africa)